

Idhini ya Kushiriki kwenye Utafiti

Neno “wewe” linalotumiwa katika hati hii linamaanisha mshiriki wa utafiti. Inamaanisha pia mtu ambaye ameidhinishwa kutoa idhini kwa ajili ya mshiriki kwenye utafiti huu.

Unaombwa ushiriki kwenye utafiti. Kabla ukubali, lazima upewe muhtasari wa taarifa muhimu ya kukusaidia kuelewa sababu zinazoweza kufanya utake ama usitake kijiunga na utafiti.

Kabla ukubali, lazima mpelelezi akuambie kuhusu:

- (i) sababu, taratibu, na muda wa utafiti;
- (ii) upasuaji wowote wa majaribio;
- (iii) hatari zozote zinazoweza kutokea, kusumbuliwa, na manufaa ya utafiti;
- (iv) upasuaji wowote mbadala unaoweza kuwa bora katika matibabu;
- (v) jinsi ambavyo mambo yako yatakuwa ya siri; na
- (vi) mtu wa kuwasiliana na yeye ukiwa na maswali, malalmiko, na majeraha

Panapohusika, lazima mpelelezi akuambie kuhusu:

- (i) fidia au matibabu yoyote yanayopatikana ukijeruhiwa;
- (ii) uwezekano wa hatari usizotarajia;
- (iii) hali ambapo mpelelezi anaweza kukomesha kushiriki kwako:
- (iv) ghamama zozote za ziada kwako;
- (v) mambo yatakayotokea ukiacha kushiriki;
- (vi) wakati ambapo utaambiwa kuhusu mambo mapya yanayoweza kubadilisha mawazo yako kuhusu kushiriki;
- (vii) idadi ya watu wakaokuwepo kwenye utafiti; na
- (viii) jinsi ambavyo unahitaji kuidhinisha matumizi ya taarifa yako ya afya kwa ajili ya utafiti.

Kushiriki kwako kwenye utafiti huu ni kwa hiari, na hutaadhibiwa au kupoteza manufaa ukikataa kushiriki au ukiamua kuacha. Kutia saini kwenye fomu hii kunamaanisha kwamba umeelezewa kwa mdomo kuhusu utafiti, ikiwa ni pamoja na taarifa iliyoko hapo juu, na kwamba umejitolea kushiriki. Ukikubali kushiriki, lazima upewe nakala ya hati hii iliyoitiwa saini na muhtasari wa utafiti uliondikwa kwa Kiingereza.

Ikiwa una maswali, malalamiko, majereha, au wasiwasi kuhusu utafiti huu, unaweza kuwasiliana na mpelelezi kwa kutumia nambari za simu zilizoko kwenye muhtasari wa utafiti uliondikwa. Ikiwa una maswali kuhusu haki zako kama mshiriki wa utafiti, au ikiwa una maswali, malalamiko au wasiwasi ambao unahisi kwamba huwezi kujadili na timu ya utafiti, tafadhalii wasiliana na Wakili wa Ulinzi wa Utafiti wa Binadamu kwa kutumia nambari za simu zilizoko kwenye muhtasari wa utafiti ulioandikwa.

Saini ya Mshiriki

Jina la Mshiriki

Tarehe/Saa (ikiwa inahitajika)

Shahidi

Kwa kutia saini kwenye fomu hii, unaashiria kwamba:

- Mshiriki huyo alipewa taarifa iliyoko kwenye Hati ya Muhtasari pamoja na taarifa yoyote ya ziada iliyosemwa na mtu anayepata idhini kwa lugha ambayo mshiriki anapendelea na anayoelewa; na
- Maswali ya mshiriki yalifasiriwa na mtu anayepata idhini alijibiwa kwa lugha anayopendelea na kuelewa.
- Katika mwisho wa mukutano wa idhini, mshiriki aliulizwa kwa lugha anayopendelea na anayoelewa ikiwa anaolewa taarifa iliyoko kwenye Hati ya Muhtasari pamoja na taarifa yoyote ya ziada yaliyoelezwa na mtu anayepokea idhini (ikiwa ni pamoja na majibu ya maswali ya mshiriki) na alikubali.

Saini ya Shahidi

Jina la Shahidi

Tarehe/Saa

Uthibitisho wa Mkalimani:

Ninathibitisha kwamba nilfasiri muhtasari kama ilivyotolewa, pamoja na maswali ya mgonjwa na majibu ya mtafiti kadri ya uwezo wangu.

Saini ya Mkalimani

Jina la Mkalimani

Tarehe/Saa